# OFISI YA WAZIRI MKUU
# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI | www.pmo.go.tz | DODOMA | TOLEO LA SEPTEMBA 2022



Katibu Mkuu
Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu
2 Barabara ya Posta 40412 Dodoma Tanzania



# SERIKALI KUJA NA MAPENDEKEZO YA SHERIA MPYA YA USIMAMIZI WA MAAFA.

Serikali imeandaa mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mpya ya usimamizi wa maafa ili kuweka mfumo wa udhibiti na uratibu wa maafa kwa ajili ya hatua za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea.

Akizungumza katika kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria iliyokutana katika Ukumbi wa Bunge Jijini Dodoma kujadili Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene alisema kutungwa kwa sheria hiyo ni kuifuta sheria iliyopo sasa ya mwaka mwaka 2015 sura ya 242.

Mhe. Simbachawene alieleza kwamba awali masuala ya maafa hayakuwa na mfumo wa kisheria wa uratibu hali ambayo imekuwa ikisababisha mgongano wa majukumu hivyo kutungwa kwa sheria hiyo kutaainisha madaraka, wajibu, maamuzi, utunzaji wa rasilimali na muono unaozingatia taarifa za hali ya hewa.

"Awali masuala ya maafa yalikuwa na daraja fulani la watu, masuala ya kisheria yalikuwa kama yako juu hata ikitokea maafa ngazi ya Wilaya au Kijiji wanasema tumuone Mkuu wa Wilaya sasa tunataka sheria iseme yanapotokea

Pia aliongeza kwamba sababu nyingine ya kutunga sheria mpya ya Usimamizi wa Maafa ni kuimarisha mfumo wa kiutendaji wakati wa maafa na upatikanaji wa taarifa na takwimu za matukio ya maafa na kuweka mfumo mpya wa kitaasisi unaozingatia mfumo wa kiutawala utakaowezesha ushiriki wa wadau wote muhimu kabla, wakati na baada ya maafa kutokea nchini..

"Eneo lingine ni kuhakikisha kamati hizi zinakuwa za kitendaji na siyo bodi ambapo itasaidia katika kutafuta ufumbuzi yanapotokea maafa pamoja na kuwezesha kurejesha hali ya awali baada ya madhara ya majanga kujitokeza," aliongeza.

Aidha alieleza kwamba utungwaji wa sheria utasaidia kutumia taarifa za hali ya hewa na majanga ambapo kamati zitatakiwa kukutana pamoja na utunzaji wa rasilimali ambazo hutumika kukabili na kurejesha hali pamoja na kuzingatia usalama wa wananchi na mali zao.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Mhe. Najma Giga aliipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuendelea kushirikiana na Kamati kuhakikisha sheria mpya inatungwa kama hatua ya kuzuia na kukabili maafa ambayo husababababisha athari kubwa.

Naye Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo Mhe. Zainabu Katimba alishauri uundwaji wa Kamati Elekezi ya Kitaifa uzingatie sekta badala ya Wizara ambayo huwa na usimamizi wa jumla wa utekelezaji wa maafa.



# JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO LAKABIDHIWA KWA WAZIRI SIMBACHAWENE

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe.George Simbachawene amepokea Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Bunge wa Saba kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Ramadhani Suleiman.

Akizungumza wakati wa kupokea Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Mhe. George Simbachawene tarehe 02/09/2022 amesema Serikali inaongozwa na sheria zinazotungwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

“Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo inaweza kutatua changamoto zote zinazogusa watu katika maswala ya sheria; kanuni, taratibu, mila na desturi zinazoongoza Serikali, alisema Waziri Simbachawene.”

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Mhe. Ramadhani Suleiman amemshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu kwa kupokea Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Saba pamoja na majibu aliyoyatoa kwa Kamati ya Bunge.



# TANZANIA YAJIPANGA KUKABILIANA NA MAAFA IKIWA NI NCHI WANACHAMA SADC.

Serikali imesema itachukua hatua madhubuti za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kupunguza shughuli zote zinazosababisha madhara ambayo yanaweza kusababisha majanga.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene Ofisini kwake Bungeni, Jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa kuhusu Mkutano wa Mawaziri wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika Msumbiji uliojadili kuhusu namna ya kuchukua tahadhari ya mapema katika hatua za kudhibiti Majanga.

Mhe. Simbachawene alisema miongoni mwa mambo waliyokubaliana ni pamoja na kuweka mifumo thabiti ya utayari kuhakikisha wananchi wanachama wanapata taarifa mapema pindi majanga yanapotokea na kudhibiti ukubwa wa madhara yake, na kuhakikisha makundi yaliyo katika hatari ya kuathirika na majanga wakiwemo Wanawake, Watoto na Watu Wenye Ulemavu wanafikiwa ili kuchukua hatua za tahadhari.

“Eneo lingine ni kuongeza uwekezaji ili kuimairisha taasisi zinazohusika na mifumo ya tahadhari za mapema na huduma za usimamizi wa maafa, kuimarisha mfumo wa kisheria wa kuziwezesha mamlaka zenye dhamana ya tahadhari kama hapa kwetu ni Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania(TMA), wanaokusanya taarifa na kuzipeleka na kushirikiana na vitengo vinavyohusika na majanga,”Alisema. Mhe. Simbachawene.

Aidha amewahimiza wananchi kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotelewa na wataalam na kuzitumia katika shughuli za kila siku pamoja na watu wanaoishi katika Ukanda wa Kusini mwa Afrika kwa kuwa na mfumo wa kubadilishana taarifa na kusaidiana kitaasisi hatua itakayosadia kuepuka majanga kabla hayajatokea.

Ikumbukwe Mkutano huo wa siku mbili ulifanyika Mjini Maputo Nchini Msumbiji ulifunguliwa na Rais wa Msumbiji Filipe Nyusi kwa lengo la kupokea maoni ya maandalizi ya maafa na namna ya kushughulikia na kutekeleza maelekezo ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guteress aliyezitaka nchi kuhakikisha raia wake wanapokea taarifa zinazoweza kusababisha majanga ikiwa ni mkakati wa kimataifa wa kupunguza madhara ya maafa ifikapo mwaka 2030.



# GLOBAL FUND YAUNGA MKONO SERIKALI KUKABILIANA NA MAGONJWA NCHINI.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. John Jingu amekutana na kufanya mazungumzo na Meneja Mkaguzi kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Kupiga Vita UKIMWI, TB na Malaria (GLOBAL FUND) Bwa. Andrew Hammond ofisini kwake Jijini Dodoma.

Dkt. Jingu amesema mazungumzo hayo yalilenga kujadili masuala mbalimbali kuhusu sekta ya afya nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya afya katika maeneo yao.

Ameongeza kuwa serikali ya Tanzania itaendelea kushirikana na mfuko huo kwani umekuwa na mchango mkubwa katika kuwezesha vifaa tiba kama ilivyo azima ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kujenga miundo mbinu ya na kuboresha masuala ya tiba kwa wananchi.

Naye Meneja Mkaguzi kutoka Mfuko wa Kimataifa wa kusaidia mapambano dhidi ya UKIMWI, TB na Malaria (GLOBAL FUND) Bwa. Andrew Hammond ameishukuru Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko huo katika kupiga vita maradhi ya Kifua Kikuu, Malaria na Ukimwi.

Ameahidi kuwa Mfuko wa Dunia utaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kukabiliana na magonjwa hayo hapa nchini kwa kuelekeza rasilimali fedha kwa ajili ya kununua dawa pamoja na kuboresha mifumo ya utoaji huduma ya afya.



# DKT. JINGU AONGOZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA TAIFA YA SENSA YA WATU NA MAKAZI

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. John Jingu ameongoza kikao cha 8 cha Kamati ya Ushauri ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi kilicholenga kupokea taarifa ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 iliyofanyika tarehe 23 Agosti, 2022 pamoja na kujadili Rasimu ya Mwongozo wa Matumizi ya Takwimu ya Sensa ya Watu na Makazi nchini.

Kikao hicho kilifanyika tarehe 27 Septemba, 2022 katika Ukumbi wa Julius Nyerere Interational Covention Centre Jijini Dar es Salaam (JNICC).

Jukumu kubwa la Kamati hiyo ni kuishauri Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa inayoongozwa na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar namna bora ya utekelezaji wa masuala ya sensa.

Jarida hili la Mtandao limeandaliwa
na kutolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu

Ofisi ya Waziri Mkuu (SBU)
Ofisi ya Waziri Mkuu (SBU)

KATIBU MKUU
Ofisi ya Waziri Mkuu
2 Mtaa wa Relini, S. L.P 980
40480 Dodoma,
Barua pepe;ps@pmo.go.tz, Simu;+255262322480
Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz